

**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO
KILICHOFANYIKA TAREHE 20/12/2021 KWENYE UKUMBI WA OFISI YA
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA MKUNWA**

WALIOHUDHURIA

1. Erica E. Yegella	Mkurugenzi Mtendaji (W)- Mwenyekiti	
2. Veronica Mwilongo	Afisa Utumishi(W)	- Katibu
3. Thomas Luambano	Afisa mipango (W)	- Mjumbe
4. Maisha S Mtipa	Kaimu Mkurugenzi (W)	- Mjumbe
5. Arthur Mbena	Mwanasheria (W)	- Mjumbe
6. Epaphroditus C. Sabuni	Afisa Mazingira (W)	- Mjumbe
7. Kassim Mbwana	Afisa maendeleo jamii (W)	- Mjumbe
8. Gerald Sasita	Kny Mratibu TASAF (W)	- Mjumbe
9. Edward Kashinye	Mkaguzi wa Ndani (W)	- Mjumbe
10. Johnia Rwebangira	Kaimu Afisa Ardhi(W)	- Mjumbe
11. Augustino Mwangosi	Kaimu Afisa Nyuki (W)	- Mjumbe
12. Isack N. Bilali	Kaimu Afisa Habari(W)	- Mjumbe
13. Hamis M. Rwambo	KNY, TEHAMA (W)	- Mjumbe
14. Dr. Innocent T.M	Kaimu DLFO (W)	- Mjumbe
15. Eng. Elias Kuyeko	Kaimu Afisa Ujenzi (W)	- Mjumbe
16. Patrick J. Almasi	Afisa Ugavi(W)	- Mjumbe
17. Scholastica Bernad	Afisa Tarafa	- Mjumbe
18. Marco Mapunda	Afisa Tarafa	- Mjumbe
19. Winifrida J. Linyembe	Afisa Tarafa	- Mjumbe
20. Efenia S. Komba	Kaimu Afisa Kilimo(W)	- Mjumbe
21. Yunus Bhatia	Kaimu Afisa Elimu (M)	- Mjumbe
22. Dr. Matayo Malaika	Kaimu Mganga mkuuu	- Mjumbe
23. Davis Kasembe	Kaimu Afisa Elimu (S)	- Mjumbe
24. Soloko shaibu N.	Mwandishi wa Vikao	
25. Zuhura Nandala	Mwandishi wa Vikao Msaidizi	

WASIOHUDHURIA

1. Doris Kavindi Afisa Tarafa - Kitaya Kwa taarifa ya Ugonjwa

MUHT. NA. 72/2021/2022. KUFUNGUA KIKAO

Katibu alimkaribisha mwenyekiti afungue kikao, baada ya akidi kukamilika. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kawaida ambacho kilitakiwa kufanyika tarehe 16/12/2021, lakini kutokana na mwingiliano wa majukumu kiliharishwa sadi tarehe 20/12/2021. Aliomba wajumbe kuchangia kwa makini ajenda zote. Baada ya maelezo hayo mwenyekiti afungua rasmi kikao saa 4:40 Asubuhi.

MUHT. NA. 79/2021/2022. TAARIFA MBALIMBALI

1) Taarifa ya uendelezaji wa kituo cha Afya Mkunwa ujenzi wa ICU na nyumba za watumishi Kilambo.
Kaimu Mganga Mkuu aliwasilisha taarifa ikieleza kuwa: Halmashauri ilipokea fedha tarehe 29/09/2021 kiasi cha Shilingi Milioni mia mbili na Hamsini (250,000,000) kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi katika kituo cha Afya Mkunwa. Majengo yaliyoelekezwa yajengwa ni Jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Kichomea taka (Incinerator) na Jengo la

**MUHT. NA. 68/2021/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA COVID 19 KIASI
CHA TSHS 1,080,000,000.00 KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA**

Afisa Mipango wa Halmashauri alitoa maelezo kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tshs. 1,080,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 50 ya sekondari na madarasa 4 shule shikizi. Alisema utekelezaji wa ujenzi wa madarasa hayo yanahitajika mapema kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022 ili kuondokana na changamoto ya madarasa. Aidha ilisisitizwa na OR- TAMISEMI kuwa utekelezaji wa mradi huu utumike utaratibu wa "Force Account."

Baada ya maelezo kuwasilishwa wajumbe walipokea kisha mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kuchangia.

Mjumbe wa kwanza alishauri fedha hizi zitumike kwa shughuli husika ili kuondokana na changamoto za madarasa.


Mjumbe mwingine alisema kwa vile ujenzi wa madarasa hayo ni ya utekelezaji wake wa muda maalum ili yakamilike alishauri kujipanga vyema ili tuendane na muda.


Mwenyekiti alisisitiza kujipanga vizuri ili kuweza kukamilisha madarasa hayo.

MUHT. NA. 72/2021/2022. KUFUNGA KIKAO

Katibu alimkaribisha mwenyekiti afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuomba kwenda kufanya kazi marekebishi yaliyoshauriwa. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 8.45 mchana.

MUHT. UMETHIBITISHWA NA:-


SAINI YA KATIBU


SAINI YA MWENYEKITI

20/12/2021

TAREHE